Muharram

ni mwezi wa kwanza katika miezi ya mwaka (wa Kiislamu) wa Hijiriya.

Maana ya jina:

Muharram ni kwa maana ya kwamba ni haramu kupigana vita katika mwezi huo, kwa sababu ni mmojawapo wa miezi mitukufu. Pia unaitwa Mwezi wa Allah kwa ajili ya kuutukuza, na pia unaitwa Mwezi Kiziwi kwa sababu ya ukubwa wa heshima yake.

Ni zipi sheria za miezi mitukufu?

Mwenyezi Mungu ameamrisha **kuadhimisha matukio yake ya ibada, kuja**li kuepuka kufanya mambo ya haramu na kujali kufanya ibada. Kufanya maovu katika miezi hiyo ni dhambi kubwa sana kuliko katika miezi mingine. *"Kwa yakini, idadi ya miezi mbele ya Mwenyezi Mungu ni kumi na mbili katika kitabu cha Mwenyezi Mungu siku alipoumba mbingu na ardhi. Miongoni mwake kuna (miezi) mine mitukufu. Hiyo ndio dini iliyo nyooka. Kwa hiyo, msizidhulumu humo nafsi zenu".* Sura Attauba (9), aya 36.

Kuanzisha vita katika miezi mitukufu ilikuwa haramu mwanzoni mwa Uislamu. Halafu sheria hiyo ilifutwa na miezi hiyo ikawa kama miezi mingine katika kupigana vita, kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa: *"Kwa hiyo, msizidhulumu humo nafsi zenu. Na piganeni vita na makafiri wote kama wao wote wanavyopigana vita na nyinyi ".* Sura Attauba (9) , aya 36. Lakini ni wajibu kwa Muislamu kuchukua tahadhari katika miezi hiyo na kujibidiisha kufuata sheria za Kiislamu kama alivyo amrisha Allah.

Na miezi mitukufu

ni miezi mine ambayo Mwenyezi Mungu ameamrisha kuiadhimisha na ni haramu humu kupigana vita ili kuwalinda mahujaji na wanaoitembelea Alkaaba waweze kufanya ibada ya Hija kwa amani na utulivu:



Huu ni mwezi wa kumi na moja. Mahujaji hujiandaa katika mwezi huu na kuanza safari ya kwenda Makka.

Huu ni mwezi wa kumi na mbili. Ndani ya mwezi huu yanafanyika matukio ya ibada ya Hija.

Huu ni mwezi wa kwanza katika mwaka, na katika mwezi huu Mahujaji wanarudi nchini mwao

Huu ni mwezi wa saba unaokuwa katikati ya mwaka ili anayetaka kuzuru Alkaaba nje ya msimu wa Hija aweze kufanya hivyo kwa amani na utulivu.

Ubora wake:

1

Ni mwezi bora zaidi baada ya mwezi wa Ramadhani, na unahusishwa kwa Allah kwa lengo la kuutukuza na kuupa hadhi. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwezi bora zaidi ya miezi mingine ni mwezi wa Mwenyezi Mungu mnao uita "Muharram".* Amaeipokea Hadithi hii Annasai katika kitabu chake cha Sunan Kubraa, Hadithi Na. 4202.

2

Funga ya saumu ndani ya mwezi huu ni funga bora zaidi baada ya mwezi wa Ramadhani. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Funga bora zaidi baada ya Ramadhani ni mwezi wa Mwenyezi Mungu wa Muharram".* Amaeipokea Hadithi hii Annasai katika kitabu chake cha Sunan Kubraa, Hadithi Na. 4202.

3

Ni mmojawapo wa miezi mitukufu, bali ni mtukufu zaidi ya wenye hadhi zaidi.

Kwa nini umekuwa mwezi wa kwanza?

Swahaba walipokubaliana mwaka wa 16 wa Hijriya katika kipindi cha uongozi wa Omar Bin Khatwab kwamba waanze tarehe kwa kuanzia mwaka aliohama Mtume (s.a.w.) (kutoka Makka kwenda Madina), walichagua kuuanza mwaka kwa mwezi wa Muharram kwa kuzingatia sababu za busara. Miongoni mwa sababu hizo ni hizi:

1 Kwamba huu ni mwezi ambao Mtume (s.a.w.) alitia azma ya kuhama baada ya kukutana kwake na Answaar pale Aqaba baada ya Hija.

2 Kwamba huu ni miongoni mwa miezi mitukufu unaokuja mara tu baada ya mwezi wa Hija. Baada ya Waislamu kukamilisha ibada zao za wajibu katika mwaka huu ikiwemo funga na Hija, inakuwa uzuri wauanze mwaka mpya kwa mmojawapo wa miezi mitukufu kama walivyo uhitimisha mwaka kwa mwezi mtukufu.

Siku ya Ashura

Siku ya Ashura imepewa jina hili kwa sababu ya kuhusishwa na namba Ashara (kumi) kwakuwa hiyo ni siku ya kumi katika mwezi wa Muharram.

Kwa nini tunafunga Ashura?

Mtume (s.a.w.) alipofika Madina aliwakuta Wayahudi wamefunga katika siku ya Ashara na kuwauliza kwamba: "Ni nini hii siku mnayoifunga?". Wakajibu kuwa: *"Hii ni siku tukufu. Mwenyezi Mungu alimuokoa Mussa na wafuasi wake katika siku hii na kumuangamiza majini Firauni na wafuasi wake, na kwa hiyo Mussa aliifunga kwa ajili ya kushukuru. Kwa sababu hiyo sisi tunaifunga".* Mtume akasema kuwa: *"Basi sisi tuna haki zaidi na tunafaa zaidi kumfuata Mussa kuliko nyinyi".* Mtume wa Mwenyezi Mungu aliifunga siku hiyo na kuamrisha watu waifunge. (Bukhariy 3943, Muslim 1130). Kwa hiyo, sisi tunaifunga siku hii kwa kumuiga Mtume (s.a.w) na kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na kumnusuru Mtume wake Mussa, Allah amfikishie amani.

Ubora wa kufunga **Ashura**

Kufunga Ashura kunafuta dhambi za mwaka mzima uliopita. Mtume (s.a.w.) amesema katika kuielezea funga ya siku ya Ashura kuwa: *"Ninataraji kwa Allah kuwa itafuta (dhambi za) mwaka uliopita".* (Muslim 1162). Inasemekana pia kwamba siku ya Ashura ni siku bora zaidi ambayo funga isiyokuwa ya faradhi inafungwa. Ibni-abbas, Allah awe radhi naye yeye na baba yake, amesema kuwa: *"Sikumuona Mtume (s.a.w.) anajali kufunga siku anayoiona bora zaidi kuliko siku nyingine isipokuwa tu siku hii ya Ashura".* (Bukhariy 2006, Muslim 1162).

Ulinganishi wa siku ya ***Ashura*** na siku ya ***Arafa***

Daraja za kufunga Ashura:

12 11 **10** 9 8

Kufunga siku ya kumi peke yake

kwa mujibu wa Hadithi zinazoelezea ubora wa funga ya Ashura kwa jumla.

12 11 **10** 9 8

Kufunga siku ya tisa, siku ya kumi na siku ya kumi na moja

kwa sababu kuna nukulu ya Hadithi iliyonukuliwa kwa Ibni-abbas kwa kuwepo kwa neno "na": *"Fungeni siku moja kabla yake na siku moja baada yake".*(Baihaqiy katika Sunan Kubraa, Hadithi Na. 8406)

12 11 **10** 9 8

Kufunga siku ya kumi na siku ya kumi na moja

Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: *"Tafautianeni na Wayahudi. Fungeni siku moja kabla yake au siku moja baada yake".* (Ahmad 2154, Ibni-khuzaima 2095)

12 11 **10** 9 8

Kufunga siku ya tisa na ya kumi

Hii ndio daraja bora zaidi, na ndio ambayo Mtume (s.a.w.) alitia azma ya kuitekeleza. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: *"Endapo nitabaki (kuwa hai) mpaka mwakani, kwa yakini kabisa, nitaifunga siku ya tisa".* (Muslim 1134) Mtume alimaanisha kuwa atafunga siku ya tisa na ya kumi.

Ashura

na kuuawa kwa Hussein, Allah awe radhi naye:

Katika siku ya Ashura mwaka 61 Hijriya (680 AD) na katika tukio baya na la kusikitisha, aliuawa Hussein Bin Ally Bin Abitwalib Bwana wa vijana wa peponi, mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, mtoto wa Fatma Azzahraa (Binti wa Mtume), mmojawapo wa Swahaba wakubwa na mmojawapo wa wanazuoni wakubwa wa Kiswahaba. Waliuawa pameja naye watoto wake wengi na watu wa familia yake tukufu. Ni msiba mkubwa ulioukumba umma wa Kiislamu kama umma huu ulivyokumbwa na misiba mkubwa zaidi kuliko huo pale Omar Bin Khatwab na Ally Bin Abitwalib walipouawa, na kabla ya hapo pale Mtume (s.a.w.) alipofariki. Hakutokeapo yeyote miongoni mwa watoto wao na wapenzi wao akakiwekea kifo chao msimu wa maombolezi na kilio. Sasa vipi leo hii kufanyike kujipiga makofi na kelele za maombolezi; mambo ambayo ni miongoni mwa madhambi makubwa?

MODERN GUIDE

Mradi: Muongozo mwepesi wa Muislamu
Usanifu: Hassan Baharoun
Utayarishaji: Shirika la Aldaliil Almuasir

Rejea:
Kitabu cha ***Lataaif Almaarif*** cha Ibnirajab
Ahkaamulqur'an cha Qurtubiy
Tafsiirulqr'an Al-adhiim cha Ibnikathiir, tafsiri ya sura Attauba ay 36-37.